**Learning by Ear – Elimu na Kazi**

**Mafunzo ya Chuo Kikuu- Hadithi ya Malaika / Episode 01**

**Mwandishi : C. Muhoho**

**Mhariri: Maja Dreyer**

**Tafsiri :Eric Ponda**

**WAHUSIKA:**

| | |
|---|---|
| Mtangazaji | : Mtu Mzima |
| Malaika | : Msichana miaka 19, amepita mtihani wake wa shule ya Msingi |
| Bi Grace | : Miaka 52- Mwalimu na mnasihi wa Malaika |
| Shangazi Tizo | : Miaka 64- Shangaziye Malaika. Ni Dada Mkubwa Mzee Nathan. Mkakamavu na mjasiri ila tu hana kisomo |
| Mzee Nathan: | Miaka 60- Babake Malaika. Mwenye kuzimngatia zaidi utamaduni |
| Mama Rose | : Mamake Malaika. Miaka 45, mtiifu na pia mwenye kuzingatia uitamaduni |
| Mzee | : Mzee wa kijiji miaka 82 |

INTRO

***MUZIKI - UTANGULIZI***

1. Mtangazaji Hujambo mpenzi msikilizaji na karibu kwa mara nyingine kwa makala ya “Learning by Ear” makala yanayozungumzia Elimu na Kazi. Katika vipindi vyetu sita vijavyo tutasikia na

kujifunza mengi kuhusu elimu, na maisha ya Chuo Kikuu.Yale yanayokupasayo kufanya kujiunga na chuo kikuu, na jinsi ya kukabiliana na masomo chuoni. Ungana nasi kwa hadithi hii kuhusu kijiji cha Kanunga.

Ni mwanzo mpya kwa msichana aliyepita mtihani wake wa shule ya sekondari.Na sio kupita tu, bali pia na kuwashinda wanafunzi wenzake wa kiume darasani. Je maisha yake yatakuwaje siku za usoni?

<u>SCENE 1:</u> <u>**KIJIJI CHA KANUNGA. NYUMBANI KWA MZEE NATHAN**</u>

SFX: ***MAZINGARA YA KIJIJI CHA KIAFRICA, NGOMBE, NA NDEGE WAKIIMBA:***

2. MZEE NATHAN: Malaika, binti yangu, umetufanya matajiri sisi wazazi wako. Mahari yako sasa yataongezeka maradufu kwa ng´ombe 10.

3. MALAIKA : (*akiwa amefurahi)* Nilijua kwamba nitapita mtihani wangu…lakini si hivi! Mwalimu Grace unahakika?

4Bi GRACE : *(akitaharuki)* Kabisa, kama vile jua litakavyochomoza kesho...! Wewe ndiye mwanafunzi bora zaidi nimewahi kufundisha shuleni.

5. MAMA ROSE: Lakini elimu hiyo inamanufaa gani kwa mtoto wa Kike? Hii si nikujiletea balaa tu binti yangu!

**SFX:** ***Akigongagonga bakora yake mahala pagumu***

6. MZEE NATHAN: AAHA BALAA…. MWANAMKE WEE, HEBU NYAMAZA! NA UANZE KUTAFUTA MCHUMBA

7. Bi GRACE : Oh, Mzee Nathan, mchumba au sanduku..!

8. MZEE NATHAN : Ebo..! Kwani wachumba wanabebwa kwa masanduku siku hizi.?

9. MALAIKA Ehh ..…sanduku la kutumia chuoni baba… mimi najiunga na chuo kikuu...!

**SFX:*GHAFLA MCHAKARISHO WA NGUO NA FANICHA*.**

10. MZEE NATHAN: Eti nini? Wasichana wa umri kama wako sasa wanaitwa mama! Chuo hicho ulikipata wapi?

11. MALAIKA : Nilikipata kwa usaidizi wa Mwalimu Grace.

12. MZEE NATHAN: Mwalimu Grace, eti ulifanya nini?

13.BI GRACE: Nilikwenda kwa ofisi za elimu na kisha nikajaza fomu za maombi ya kujiunga na chuo kikuu cha umma jijijni. Na kisha ili kuhakikisha kwamba hatukosi nafasi hiyo, nikatafuta nafasi katika vyuo vingine vya

kibinafasi kupitia mtandao wa Intaneti hapa mjini.

14.MZEE NATHAN: Hukupasa au hata kufikiria hivyo, wewe….!, ***(anakatizwa)***

***SAUTI YA MWANAMKE AKIIMBA NA KUPIGA VIGELEGELE INAKARIBIA*.**

15. SHANGAZI TIZO: Allillillillillilli!!!! hererere…hererere ..hererere... Kijiji kizima sasa kinasherehekea na kumpongeza binti yetu! Kumpongeza binti aliyeshinda kila mmoja shuleni hata wavulana… herere hererere…hererere!!!!!

16. MZEE NATHAN: Dada Tizo, wacha kusherehekea, anataka kujiunga na … na .. na ..chuo kikuu.

17. SHANGAZI TIZO:***(Amesisimkwa)***, Kakangu, ni vile tu mimi sikuzaliwa mwanamume, mimi ni mkubwa wako, na ningekwambia ufunge domo lako.

18. MZEE NATHAN : Hebu nyamazeni, mnanisikiliza?,… Mama , nenda ukawaite wazee wa kijiji haraka! Ni lazima tumtafutie mchumba huyu binti yetu kabla hajakorogwa akili.!

19. MAMA ROSE : Binti yangu Malaika,… sikiliza ushauri wa babako!.

20. MALAIKA : Lakini nataka kuwa mhandisi na mtaalamu wa kilimo.

21. SHANGAZI TIZO: Lakini hayo si ni masomo ya wanaume?

22. Bi GRACE : Siku hizi, wasichana wanaweza kusomea taaluma wazitakazo. Mfano, wakati mimi nilipandishwa cheo na kuwa mwalimu mkuu, wengi walisema kuwa mwanamke hafai kuwa mwalimu mkuu. Lakini si nimefaulu..na hata kumtoa mwanafunzi bora zaidi?

23. MZEE NATHAN : (***kwa ugomvi***)

Tosha, tosha…., kwanza hatuna pesa hizo. Mazao hayakufanya vyema msimu huu kwa sababu ardhi imechoka haina rotuba ya kutosha, nao ngombe wetu pia hawatoi maziwa siku hizi.

24. MALAIKA : Baba hii ndiyo sababu nataka nisomee masuala ya kilimo. Nitasaidia kuistawisha ardhi yetu na kuongeza kiwango cha utoaji maziwa kwa ng´ombe wetu na….

25. SHANGAZI TIZO : Kakangu, hebu itisha kikao cha baraza la wazee hapa, maana tunajukumu kubwa la kumpeleka msichana wetu chuo kikuu.

26. MZEE NATHAN Hasaaaa, kikao hicho kinapasa kuitishwa haraka ili tumtafutie mchumba binti yetu.

***MUZIKI:***

SCENE 2: ***KIKAO CHA BARAZA LA WAZEE***

**SFX: *MAZINGARA YA KIAFRICA JIONI:WIBARI; NGOMBE WAKIKAMULIWA, SAUTI YA MOTO UKIWAKA, NA WAZEE WAKINONG'ONA*.**

27.MTANGAZAJI : Sasa wazee wamekutana, kama kawaida kuchanganua changamoto zinazoikabili jamii. Suala hilo limekuwa likijadiliwa kwa muda na sasa ni sharti lipate ufumbuzi .

28. MZEE : Tusikizane, tusikizane jamani!…. Tumekubaliana kwamba endapo msichana huyu atapata elimu zaidi, basi atakuwa wa manufaa makubwa kuliko mahari.. Mzee Nathan, unaweza kusubiri miaka michache tu ijayo kisha tutapata……

SOUND: ***Wazee wanong`ona kwa makubaliano***

29.MZEE NATHAN : Lakini mimi na wewe hatuna hizo pesa. Elimu ya chuo kikuu ni ghali mno! Mazao yetu hayakufanya vyema, na ng`ombe nao….

30.MZEE : (**akimkatiza***)* Kwani unasau kidole kimoja hakiwezi kuua chawa?

*(**akiwageukia wazee**)* Nendeni mukatafute michango, kila mmoja alete mchango wake hapa, kisha tuandae harambee kubwa kuchanga pesa.

***SOUND: WAKIPIGA MAKOFU KUUNGA MKONO MAPENDEKEZO*.**

***MUZIKI***

**<u>SCENE 3: *UWANJA WA KIJIJI KWA HARAMBEE YA KUCHANGA PESA :*</u>**

31.MTANGAZAJI : Siku imewadia kwa wanakijiji kutoa michango yao kumwezesha msichana huyo kujiunga na chuo kikuu. Kila mmoja ameleta mchango wake au mali ya kunadiwa..

32.MZEE : Jogoo mmoja,…mkubwa anawika kila alfajiri…! Shilingi 100 tu!.

33.SAUTI : Shilingi 120

34. MZEE Mimi nitamununua kwa 150… Elimu ya chuo kikuu si rahisi eti…!

35. SAUTI Shilingi 200...

36.MZEE : Sawa, shilingi 200 kwa mara ya kwanza, 200 kwa mara ya pili……lete pesa.

***SOUND: NYUNDO YA MBAO IKIGONGWA MEZANI.***

37. MZEE : Nyingine…. gunia la mahindi….. nitalinunua kwa shilingi 20, nani ananipinga? ***(sauti ikitokomea)***

38.MTANGAZAJI : Licha ya juhudi za kuuza mali waliyonayo, kuku na mazao, juhudi hizo zinaonekana kugonga mwamba kwani hawajafikia hata nusu ya pesa zinazohitajika chuoni. Na sasa ni lazima watafute njia nyingine.

**SAUTI:** ***PESA ZIKIHESABIWA.***

39. Bi GRACE : ***(hajaridhika)*** Hazitoshi….!

40. MALAIKA : ***(akivuta makamasi kwa hasira)*** Sasa tufanyeje?

41. BI GRACE : Mungu atatupa njia.

42.SHANGAZI TIZO : ***(akimugeukia Bi Grace)*** Mwalimu Grace nimekuona ukienda benki mara kwa mara.

43. Bi GRACE : (***kwa tahadhari***) Ndio. Kwa nini?

44. SHANGAZI TIZO: (***akishupalia)*** Unaweza kutukopesha.

45. MALAIKA : ***(ataharuki)*** Tafadhali,.. tafadhali Mwalimu. Nitakufanyia kazi… nitakufanyia kazi wakati wa likizo…..kweli….!

46.BI GRACE : Lakini si itakuwa kazi nyingi kwako!

47. MALAIKA : Nakuahidi Mwalimu Grace. Nitajaribu kutumia elimu yangu chuoni kuboresha kilimo hapa kijijini, kuimarisha uzalishaji na kisha nitaweza kulipa mkopo wako kutoka kwa pato langu. Kwa kufanya hivyo kila mmoja wetu hapa kijijini atanufaika, mavuno yataimarika, wewe utakuwa umefanikiwa kumpeleka chuoni mwanafunzi wako bora, nami kusomea kilimo chuoni.

48. BI GRACE : Mungu kweli hutimiza mahitaji yetu…!

***MUZIKI***

OUTRO

49. MTANGAZAJI

Malaika sasa amefanikiwa kuruka kizuizi cha kwanza baada ya babake kushawishika ajiunge na chuo kikuu badala ya kuolewa. Pia amepata mkopo kugharamia masomo yake kwa mhula wa kwanza. Changamoto kubwa sasa ni jinsi atakavyofika jijini na kusoma kwa bidii ili kuinufaisha jamii yake nyumbani,ambayo imemsaidia sana kufanikisha azma yake ya kujiunga na chuo kikuu. Je Malaika

ataweza kumudu changamoto hizi? Ungana nasi kwa makala nyingine ya `Learning by Ear` jenga maisha yako, kuhusu elimu ya chuo kikuu. Pia unaweza kutembelea mtandao wetut www.dw-world.de/lbe ili ujifunze mengi zaidi. Kadhalika unaweza kututumia maoni yako kuhusiana na vipindi hivi vya Learning by Ear. Hadi wakati mwengine. Kwa heri.